

## Hatua ya saba

Fungua mfuko na kuanza kuwalisha baada ya juma moja hadi mbili. Katika sehemu zenye baridi kama vile Nyandarua, fungua baada ya majuma matatu.

## Gharama ya kukutayarisha

- Gharama ya kutayarisha kilo 100 za masalio ya mahindi ni shilingi 450 za Kenya (Bei ya Disemba 2007).

## Faida za masalio yaliyoongezewa mbolea

- Mifugo hutoa maziwa mengi na hukua haraka.
- Majani yaliyotayarishwa hivyo yanaweza kutumika badala ya nyasi za kizungu.
- Wakulima hupata pesa nyingi.
- Mifungo wanaolishwa chakula hicho hutoa samadi/ mbolea ya thamani ya juu.

## Uwezo wa mifugo

Uwezo wa mifugo waliolishwa majani hayo yaliyotayarishwa hivyo pamoja na majani ya mifugo kama lucerne na majani ya viazi vitamu huwa ni sawa na ule wa mifugo waliolishwa nyasi za kizungu.

## TAHADHARI

\* USITHUBUTU KUWALISHA MIFUGO MBOLEA HIYO YA UREA IKIWA CHEMBECHEMBE AU BAADA YA KUCHANGANYWA NA MAJI. INAWEZA KUWA SUMU AU KUSABABISHA TUMBO KUVIMBA NA HATIMAYE VIFO VYA MIFUGO.



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

### Mtayarishaji:

Kiruiro, E.M.

### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Embu

S.L.P.27 Embu

Simu 06820116/20873 nukulisi 068-30064

Baruapepe: kariembu@salpha.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 19 /2008

**Shilingi Ishirini za Kenya**

# Jinsi ya kuboresha masalio ya mimea ili kuilisha mifugo



## Utangulizi

Masalia ya mimea kama vile mihimili ya mahindi, ngano na mchele hupatikana tele wakati wa kiangazi. Hata hivyo masalia haya yana kiwango duni cha protini na hayasagiki vizuri tumboni mwa mifugo.

Kiwango cha masalia haya kinaweza kuboreshwa kwa kuongezewa mbolea ya kawaida.


## Hatua za kutia mbolea

### Hatua ya kwanza

Kata kata masalia ya mimea kwa kutumia panga au mashine.

### Hatua ya pili

Pima kilo 100 za masalia yaliyokatwakatwa na uyatandaze kwa karatasi ya plastiki.



Kuyapima majani



Ndoo ya maji

### Hatua ya tatu

Weka kati ya lita 4 hadi 5 za maji kwenye ndoo ya maji kisha upime gramu 400 hadi 500 za mbolea aina ya urea na uchanganye na maji (mbolea ya urea huchanganyika mara moja).



Kunyunyizia mseto kwenye majani

### Hatua ya nne

Nyunyizia mseto huo kwenye majani yaliyotandazwa kwenye plastiki na uchanganye vizuri kwa kutumia mikono au kijiko cha mchanga.

## Hatua ya tano

Yatie majani kwenye mfuko wa plastiki ngumu yenye upana mkubwa (kiwango cha kati ya mita 1.5 hadi 2 kilichofungwa upande mmoja na kamba za mkonge).



Kujaza na kushindilia majani katika mfuko wa plastiki

### Hatua ya sita

- Rudia hatua ya 2,3,4, na 5 hadi mfuko ujae kabisa.
- Kisha ufunge mfuko na kuhakikisha hauingizi wala kupoteza hewa. (mfuko wa mita 1.5 hadi 2 unaweza kubeba kilo 150-200 za chakula hicho cha majani).



Chakula kwenye mfuko wa plastiki